



**Kijitabu hiki ni Maalum kwa ajili ya kuzienzi, kuheshimu na kuendeleza fikra za
Marehem Daud Mwangosi.**

**Yeyote anunuaye kijitabu hiki anachangia asilimia tano (5%) kwa familia ya Marehemu
Daudi Mwangosi**

Rasimu ya kitabu sio kitabu © 2014 Justin Mpotwa

SHUKRANI

UTANGULIZI

Nilikuwepo, nilimwona lakini sikumtambua mpaka pale nilipoelezwa ameuawa. Kweli inasikitisha, inatisha pale unapoambiwa kuwa mmoja ya wale mliokuwa nao dakika takribani tano tu zilizopita, akiwa mzima, mcheshi, mchapakazi na mwenye nia ya kuleta Mabadiliko kuwa sasa hamtakuwa nae milele. Hapa ninamzungumzia Daudi Mwangosi, mmoja ya waandishi wa habari ambaye maisha yake yalikatika ghafla akiwa kazini tena chini ya vyombo vya dola ambavyo moja ya jukumu lake ni kuhakikisha linalinda uhai wa wananchi wake.

Ninayeandika haya, ndie niliyeandika barua ya kuitaarifu serikali kuhusu shughuli za CHADEMA. Ninaitwa JUSTIN LEONARD MPOTWA. Wakati wa kifo cha Daudi, mimi nilikuwa Katibu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) wilaya ya Mufindi.

Mpaka siku ya tukio, sikuwa ninamfaham Mwangosi, Daudi kwa sura ila niliwahi kuzisikia sifa zake. Siku ya tukio nilimwona Mwangosi takribani dakika tano kabla ya tukio la amri ya aliyekuwa Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Iringa, bwana Kamuhanda (RPC), Kutoa amri ya kututawanya na kuwakamata viongozi wa CHADEMA.

Ningependa niwaambie umma wote utakaosoma kijitabu hiki kuwa Sisi CHADEMA hatukutenda kosa lolote kuendesha shughuli za chama wilayani Mufindi na hasa pale Nyololo, kikatiba na kisheria. Pia vile vile ningependa niwaambie umma kuwa Mwangosi aliuawa na polisi mbele ya Kamishna wa Jeshi la polisi wa mkoa wa Iringa wakati huo na sio kama ilivyokuwa imetangazwa awali na shirika la Utangazaji la Tanzania (TBC) kuwa mwangosi aliuawa na kitu kizito toka kwa wanachama wa CHADEMA.

Zaidi ya hayo, ningependa niwaambie umma, kuwa serikali ya mkoa wa Iringa haijawahi kukiri kuhusika na kifo cha Mwangosi zaidi ya kunyoosha kidole kwa CHADEMA ambao kinyume

chake walijihusisha moja kwa moja hata katika shughuli za Msiba wa Marehemu. Serikali ya mkoa wa Iringa haijawahi hata kutoa rambi rambi kwa familia ya marehemu.

Mwisho kabisa, ningependa kuzipongeza jamii mbalimbali zilizoonyesha kuguswa na jambo hili ikiwemo waliojitoa kuona nini kilitokea, nani alikuwa anahusika, nani mwenye makosa na nai alitakiwa afanye nini ili kuzuia kile kilichotokea. Hata hivyo ninasikitika kwa baadhi ya ripoti zilizotolewa na baadhi ya tume zilizoundwa kuchunguza undani wa tatizo, hasa ripoti ya tume ya jaji Ihema. Hata hivyo ninaipongeza Tume ya Haki za binadamu. Ninayasema haya kwa kuwa mimi ni shahidi wa moja kwa moja wa kile kilichotokea, kabla, wakati na baada ya kifo cha Mwangosi. Ushahidi mwingine ni walakini..

Nikiri kuwa Pamoja na kuwa nilihojiwa na tume ya Jaji Ihema, nikaeleza ukweli na nikatoa Mapendekezo lakini nilisikitishwa na mapendekezo yaliyotolewa na tume hii ilioundwa na serikali kama mwavuli wa kujichunguza yenyewe, hasa kwa vyama vya siasa. Ninakomelea na kuipongeza zaidi Ripoti ya Tume ya Haki za Binadamu kuwa ni sahihi kwa kuwa pamoja na kuwa sikuwahi kuhojiwa na Tume hii lakini mambo yalivyoelezwa, ndivyo yalivyo na yanatia moyo hasa kwa sisi tunaotafuta haki kwa wale wasioweza kujitafutia haki zao.

Katika kijitabu hiki, nitaandika machache juu ya Daudi Mwangosi, kwa namna ambavyo nilipata kumfahamu katika dakika zake tano za mwisho hapa duniani. Kama nilivyoeleza awali kuwa nilipata kumsikia tu Mwangosi na sikuwahi kumwona kabla ya siku ya tukio. Nilimfahamu siku ya tukio muda mfupi kabla ya kufa kwake. Ni sentensi moja iliyoweka muhuri wa kumbukumbu yake ndani ya moyo wangu, **“niliyokueleza ofisini, bado hujatosheka nayo?”** Ni maneno aliyotoa Kamuhanda kwa Mwangosi na baada ya hapo hawakuwahi kuongea tena. Nitatoa sifa tano za Mwangosi ambazo ndizo nguzo za tabia ya Mwangosi na pia zinapaswa kuwa sifa za wanaharakati wote ikiwemo mimi. Kila sifa nitakayoieleza, naomba isimame kwa heshima za

Rasimu ya kitabu sio kitabu © 2014 Justin Mpotwa

kila dakika katika dakika tano za mwisho za uhai wa Mwangosi. Ni kama vile ninatafakari kwa kina kila dakika ya Mwisho ya Uhai wa Mwangosi nikihusianisha tabia yake katika kuipigania Jamii.

Samahani kwa wale ambao ninawataja katika kijitabu hiki kana kwamba wao wanasifa mbaya, hapana. Ila tu sina namna kwa kuwa wanahusika moja kwa moja na yaliyotokea na zaidi ya hayo sijaona wakichukuliwa hatua badala yake kupewa zawadi na kupongezwa wazi wazi. Sikuwa nimepanga kuandika hiki lakini kwa kuwa nimengoja toka Mwangosi afariki kuona nini kinatendeka juu ya haki za Mwangosi lakini sijaona kama kweli kuna utashi wa dhati juu ya Jambo hili.

Ningependa niwatie moyo wanaharakati wenzangu wote. Kazaneni, kazi bado ipo na tusife moyo.

Kwa wasomaji na watakapo nunua hiki kijitabu, mnachangia asilimia 5% kwa familia ya Mwangosi. Nimepata wazo la kuandika kijitabu hiki kwa kuwa nilimwona, nikamfahamu Mwangosi japokuwa ni kwa muda mfupi. Hii inatosha kumwelezea kwa vile nilivyomtambua. Hivyo sitakuwa na shukrani kama sitatoa shukrani kwa waliomfanya awe Mwangosi. Ninafahamu kuwa Marehemu ana familia ambayo ilikuwa inamtegemea na ninajua uchungu ambao wanaupata kwa kumkosa Mwangosi. Mungu aitie nguvu familia ya Marehemu hasa mke wake na watoto wake.

MPOTWA, Justin Leonard.

Yaliyomo

I. Katikati ya Wengi - alijitokeza na kuwa wakipekee

II. Katikati ya Hatari - hakuogopa

III. Katikati ya Mvutano – alitafuta Ukweli

IV. Katikati ya Amri kutoka Dola – aliendelea kutimiza wajibu wake

V. Katikati ya Wahitaji - aliwapigania

I

KATIKATI YA WENGI

“Alijitokeza na kuwa wa Kipekee”

Mwangosi, mwenyekiti wa klabu ya waandishi wa habari mkoa wa Iringa ndiye aliyeuawa pale Nyololo-mkoani Iringa. Kweli huwezi kuamini. Lakini ndiyo yaliyotokea. Tumezoea kuona viongozi wetu, wakitekeleza majukumu yao nyuma ya migongo ya walio chini yao. Hata hivyo Daud, hakufanya hivyo. Alitangulia mstari wa mbele na sasa amethibitisha kuwa yeye alikuwa kiongozi, mwenyekiti.

Tujiulize, kwa nini Mwangosi ndiye alieyekuwa kafara ya waandishi wa habari? Kuna mawazo yananjia kuwa Kifo cha Mwangosi hakikuwa cha bahati mbaya kwa maana alikuwa anavitambulisho vyote vya kumtambulisha kuwa yeye ni mwandishi wa habari. Sitaki kumnyooshea mtu kidole, lakini naamini kuwa kifo chake hakikuwa cha bahati mbaya. Kama kilikuwa cha bahati mbaya, basi waliohusika wathibishe kuwa kifo chake kilikuwa cha bahati mbaya.

Jambo la msingi zaidi kwangu ni kuona namna ambavyo huyu mwenzetu, kiongozi wetu alivyoweza kuwa kiongozi kafara. Mwangosi, alikuwa wa kipekee. Katika kuchagua jina la kijitabu hiki, haikuwa rahisi kwani ilihitaji nitafakari kwa kina sana. Nafahamu hatari iliyopo mbeleni lakini nami napenda kuungana na ndugu yangu Mwangosi kumfuata mfano wake na kuwa wakipekee.

Kwa mara ya kwanza nilimfahamu Mwangosi siku ile ile ya tukio la mauaji yake pale alipomusihi aliyekuwa kamishna wa Jeshi la Polisi mkoani Iringa amtofautishie tofauti kati ya mikutano ya ndani ya chama cha siasa na mikutano ya nje ya chama cha Siasa. Wakati huo tulikuwa tunafungua ofisi ya tawi katika moja ya ofisi hapo Nyololo pamoja na kusimika uongozi wa chama katika tawi hilo. Nitasimulia mazingira yalivyokuwa katika mada inayofuata lakini ninachoweza kukumbuka ni lile jibu alilopewa na Kamishna wa Jeshi la Polisi. Aliambiwa, ***“niliyokueleza ofisini, bado hujatosheka nayo?”*** naye akamjibu, ***“Sijatosheka, na ndio maana nipo hapa kutafuta tofauti ya mikutano ya ndani na ya nje ya Chama cha Siasa”***.

Alikuwa wa kipekee, alikuwa shujaa. Tukio hili ndilo lililonifanya mimi nimfahamu na nikagundua kuwa Kaka yetu huyu, kumbe alikuwa tayari kishafanya juhudi ya kuutafuta ukweli.

Kila mwanaharakati, ni lazima afuate nyayo za Mwangosi, au aende zaidi yake. Kuutengeneza upekee sio kazi rahisi na inahitaji sadaka ya majitoleo. Kwanza kabisa tutambue kuwa kila mmoja wetu ni wa kipekee lakini watu wengi hubaki wa kawaida sana kwa kuwa wameshindwa kufanya juhudi ya kuuonyesha upekee wao. Mwangosi alifanya juhudi kutuonyesha kuwa alikuwa wa kipekee. Na hii ndio sifa kubwa ya Mwanaharakati yeyote.

Tunawatu wanajiita wanaharakati wa kijamii hata hivyo bado wameshindwa kuuthibitisha ulimwengu kuwa wao ni wa kipekee. Kujiita mwanaharakati na kutotimiza nguzo moja wapo ya uanaharakati ni sawa kutwanga maji kwenye kinu. Harakati zozote ni lazima ziwe na utofauti na harakati nyingine. Mwangosi alikuwa shujaa.

Katika mazingira tuliyokuwepo, sitaacha pia kuwapongeza wale waandishi wa habari wengine waliokuwa na Mwangosi. Pamoja nae wanastahili kuitwa mashujaa. Tulikuwa katika mazingira ya hatari sana. Ninakumbuka tulikuwa tumezungukwa kila mahali na askari wenye kila aina ya silaha. Kifo kilikuwa kinamfuata karibu kila mtu aliyekuwepo pale lakini hasa waandishi wa habari kwani wao walikuwa wakifanya juhudi kuandika na kupiga picha kila tukio lililokuwa linaendelea. Tutapata kuiona hatari ilivyokuwa, hapo mbeleni kwenye mada zinazofuata na tutaijadili ile hatari. Tunaikosa kazi ya mwisho ya Mwangosi, kwani Kamera yake na kompyuta yake vyote vilikufa nae wakati alipolipuliwa na lile bomu. Natamani tungekuwa angalau tulibakiwa na Kazi yake ya mwisho.

Uana harakati ni kutenda. Tunahitaji watendaji. Mwangosi alikuwa kijana mwenzetu lakini tofauti yake ni kuwa alikuwa mtendaji. Tunahitaji vijana watendaji. Jamii yetu inavijana wachache ambao ndio wanafanya kila liwezekenalo kuleta mabadiliko. Wengi wa vijana si

watendaji. Jamii yetu inawanaharakati wazalendo wachache na ambao wana nia ya dhati ya kuleta mabadiliko na wenye nia ya dhati ya kutoa mchango kwa jamii. Vijana wengi hawapo tayari kujitolea. Mwangosi alikuwa mtu wa kujitolea. Hii ndio tofauti yake na vijana wengi.

Ukweli ni kuwa wote sisi tunadeni kubwa ambalo ni kuonyesha utofauti chanya kwa jamii. Hilo ni deni ambalo kila mmoja wetu atatakiwa kujibia itakapofika wakati. Mwangosi alishamaliza kazi yake na ametoa mchango mkubwa kwa jamii. Alitaka kujua tofauti kati ya Mikutano na shughuli za ndani za Vyama vya Siasa na Mikutano na Shughuli za nje za Vyama vya Siasa kisheria, Swali ambalo Kamuanda alishindwa kumjibu. Naamini Kamuanda siku moja atalijibu hilo swali.

Ni lazima tufanye juhudi kutafuta suluhisho kwa maswali magumu au matatizo makubwa ya kijamii. Ndugu yetu ametoa mchango mkubwa sana kwa Demokrasia ya Tanzania. Ningetamani awepo aje ayale matunda ya kazi zake lakini tunamshukuru kwa kuwa mchango wake utabaki katika akili zetu na tutauenzi milele. Jina lake halitafutika kamwe katika akili za watanzania na litaendelea kudumu.

Unayesoma kijitabu hiki jiulize swali, “Mimi ni nani?” Jiulize tena, “Mimi ni mwanaharakati wa Mabadiliko chanya ya kijamii?” Jiulize tena, “Mimi ni mwanaharakati wa kipekee kwa jamii yangu?” na zaidi kabisa, Jiulize, “Mimi nimeleta tofauti yeyote katika Jamii yangu?” Kama majibu ni ndio, basi Ubarikiwe sana kwa kuwa unatimiza wajibu wako kiasilia na kama hapana anza sasa kutimiza wajibu wako.

Mwangosi alijitoa. Alikamilisha wajibu wake. Hana hatia kwa asili kama alivyokuwa ametumwa. Katimiza wajibu wake na ametuachia somo la kujifunza. Tusieme kuwa sisi ni wanaharakati kama hatupo tayari kufuata mfano wa ndugu yetu Mwangosi. Kujitoa kwa ajili ya

Rasimu ya kitabu sio kitabu © 2014 Justin Mpotwa

maslai ya jamii inauma na inaumiza lakini matunda ya kile tunachokifanya ni kupata jamii iliyostaarabika.

Kumetokea watu kuanzisha vikundi, asasi au taasisi zinazojisema kuwa nazo ni za kiharakati na pale panapotokea vitisho basi hurudi nyuma. Hicho si kitendo cha kiharakati na ningependekeza kuwa yeyote anayefikiri kuwa jamii inahitaji wanaharakati waoga basi anakosea sana. Wakati fulani nimekuwa ninapendekeza kuwa wanaharakati wanapaswa zaidi kujikita katika kuiachia jamii mawazo ambayo yataibadilisha na kuiendeleza tokea pale ilipo kuelekea utimilifu au maendeleo. Wanaharakati wanaojikita katika maslai yao binafsi, wanashindwa kuitendea haki jamii.

II

KATIKATI YA HATARI

“Hakuogopa”

Labda nieleze sasa namna mazingira yalivyokuwa dakika tano kabla ya kifo cha Mwangosi. Tulikuwa tumetoka kufungua ofisi ya tawi la hapo Nyololo na sasa tulikuwa katika ofisi ya Kata ya Nyololo. Mwangosi na waandishi wenzake kama kawaida yao walikuwa wakiendelea kuchukua matukio mbalimbali.

Hapa napenda kila msomaji aungane nami kuwa wote tunafaham namna tunavyokiogopa kifo. Naamini kuwa kama Mwangosi angetambua kuwa zimebaki dakika chache baadae, hatakuwepo duniani basi pengine asingelikuwa tayari kuendelea kuwepo pale. Mwangosi angelijua hili angekuwa mbali pengine na Polisi. Hata hivyo Mwangosi aliendelea na jukumu lake la kulumikwa taifa.

Wanachama wa Chadema, walikuwa wamekaa chini kusikiliza maelekezo ya viongozi wa Chadema. Wakati huo viongozi wa Chadema walikuwa ndani ya chumba cha ofisi wakitia saina katika kitabu cha Wageni. Nje ya jengo la ofisi, Kamanda wa polisi, wa mkoa wa Iringa aliendelea kusisitiza kuwa wanachama wa Chadema watawanyike.

Nakumbuka baadhi ya wanachama na viongozi wa Chadema wakiwa na vitambaa vyeupe vikiwa vimenyanyuliwa hewani . Alama ya kitambaa cheupe hutumika na watu mbali mbali duniani kama alama ya kuonyesha Amani au kutaka Maridhiano. Fikiria, watu wamekaa chini, wakiimba nyimbo za kuhamasisha amani na utulivu na wakati huo huo wamebeba vitambaa vyeupe.

Nakumbuka, baadhi ya askari wa kutuliza ghasia wakimfuata kamanda wa polisi wa mkoa kumsisitiza atoe amri ya kutupiga. Kuna mmoja alidiliki kusema kuwa, “turuhusu tuwapige, wametuchosha hawa”. Hapakuwa na mazingira mazuri kabisa kwa waandishi wa habari na pia kwa wanachama wa Chadema. Pamoja na mazingira ya hatari, waandishi wa habari akiwemo Mwangosi waliendelea kutekeleza majukumu yao.

Ndani ya kijitabu hiki, ningependa kuwapongeza, kuwashukuru na kuwatia moyo wanaharakati wote wanaofanya kazi katika mazingira ya hatari wakiwemo waandishi wa habari.

Tumeshuhudia matukio ya kuwadhuru wanaharakati mbali mbali wakiwemo waandishi wa habari. Kwa mifano tu, tunao bwana Saed Kubenea ambaye alimwagiwa tindikali, Dr. Ulimboka aliyepigwa sana, akang'olewa kucha na meno na kutupwa katika msitu wa Mwabepande. Pia tunamkumbuka na kumtia moyo bwana Salum Kibanda ambaye yeye alipigwa na kutobolewa jicho lake.

Napenda kuwaasa watanzania wenzangu. Mazingira ambayo wanayapitia wanaharakati wengi na hasa wale wanaogusa mamlaka ya watawala ni ya hatari sana. Napenda pia kuwaasa watanzania kuwa hakuna hata mwanaharakati mmoja ambaye anapenda maisha yake yakatishwe ghafla. Ni vile tu kuwa wanaharakati wengi wanajitolea kwa kuwa wanamapenzi na wanaguswa na matatizo ya watanzania wenzao.

Kwa wale ambao hawakuwepo eneo la tukio siku ambayo Mwangosi alifariki, au kwa wale ambao hawakuwepo maeneo ya matukio mengine ya mauaji ya Raia wa Tanzania tena mbele ya macho ya polisi wao ambao mishahara yao inatokana na kodi za hao wananchi, ni lazima wote tuungane na kusema sasa basi. Inatosha.

Shughuli za kidemokrasia hazina budi kufanywa kwa misingi ya kisheria. Hilo halipingiki. Ila vyombo vya dola pia vinapaswa kutoa ushirikiano wa kisheria katika kuhakikisha demokrasia inakuwa. Mabavu ya kutumia nguvu kubwa pasipo na uhitaji ndio imepelekea raia wasio na hatia maeneo mbali mbali ya Tanzania kuuawa.

Katika kijitabu hiki pia nitaonyesha namna ambavyo serikali ilikosea na ingekuwa ni vyema hatua za kisheria zichukuliwe kwa wale waliohusika na ukiukwaji wa sheria siku ambayo Mwangosi aliuawa. Hatuna budi kuwa mashujaa kama ambavyo mwenzetu Mwangosi alifanya. Tunafanya haya kwa kuwa ni dhahiri kuwa Mwangosi alifanya kazi yake katika mazingira ya hatari na akauawa pamoja na kuwa alikuwa na vitambulisho vyote vinavyomwonyesha kuwa yeye ni mwandishi wa habari.

Niwatie moyo wanaharakati wenzangu, kuwa kazi yetu ni ya hatari sana na inahitaji moyo wa chuma. Kweli mara nyingi tumetishiwa sana. Ni wangapi kati yetu tumesita hata kujumuika na rafiki zetu mbali mbali tukihofia hatari iliyopo mbele yetu. Tukaze moyo konde na tuendeleo kuzitetea haki za raia wenzetu ambao hawana uwezo wa kupaza sauti zao.

Watanzania wenzetu tunaomba mtambue kuwa tunapitia kipindi kigumu sana katika kuwatetea haki zenu. Tunaomba msitukatishe tamaa kwa kuwa tumekuwa tukishuhudia baadhi yenu mkitukejeli na kutusimanga pale tunapopatwa na matatizo. Wengine wenu husema kuwa sisi ni nani hata tushindane na nguvu ya dola! Wengine hutukejeli kwa maneno ya kuwa eti sisi tunajifanya wambea kuikosoa serikali. Jambo hili kwa namna moja ama nyingine hutufanya tujione kuwa mnatuacha peke yetu.

Hata hivyo tunawaahidi watanzania wenzetu kuwa hatutakoma kamwe. Tutakuwa mstari wa mbele kuzipigania haki zenu hata pale mtakaposhindwa kutupa ushirikiano. Ni jambo la heri sana kufanya kazi bila kuogopa na mwisho wa siku kufikisha ujumbe wa matumaini kwa watanzania.

Wakati unafika sasa, serikali ikitaka kuaminika isijiingize katika mtindo wa kuendesha mambo yake kwa kuwatengenezea mazingira ya hatari wanaharakati mbali mbali wa haki za binadamu. Kuna baadhi ya kauli ambazo zimepatwa kutolewa na baadhi ya viongozi ambazo zimetengeneza mazingira ya hatari kwa wanaharakati mbali mbali. Baadhi ya kauli zilitolewa ufafanuzi, nyingine kuombewa msamaha lakini nyingine licha ya kutengeneza utata mkubwa hazijatolewa ufafanuzi wala kuombewa msamaha. Tunapata taabu kuamini kuwa kweli serikali ipo na nia ya dhati ya kuwapigania wanaharakati na kufanikisha kuijenga demokrasia na kuimarisha ustawi wa kijamii.

III

KATIKATI YA MVUTANO

“Alitafuta Ukweli”

Hapa sasa nitaeleza kinaga ubaga nini kilitokea kabla ya siku ya tukio la Mwangosi kuuawa. Chama cha Demokrasia na Maendeleo kilikua katika operesheni inayoitwa Vuguvugu la Mabadiliko (Movement for Change-M4C) ambalo lilikuwa limeanzia Lindi na Mtwara, Morogoro na sasa vuguvugu hili lilikuwa limeingia katika mkoa wa Iringa.

Mnamo tar 27/08/2012 Chadema kiliandika barua ya kulitaarifu jeshi la polisi juu ya mikutano ya hadhara ambayo ingefanyika katika wilaya ya Mufindi kwa kuwa ndiko ambako vuguvugu hili limeanzia katika mkoa wa Iringa. Tar 28/08/2012 serikali iliwasihi Chadema kusitisha mikutano ya hadhara kwa kuwa wakati huo ilikuwa ni wakati wa zoezi la Sensa ya watu iliyokuwa inaendelea nchi nzima. Zoezi hilo la Sensa lilikuwa ni la siku nne na lilikuwa linaishia tar 01/09/2012.

Chadema ilikubaliana na mapendekezo na kuamua kufanya shughuli za ndani za Chama. Chadema ilikubaliana na polisi kusitisha mikutano ya hadhara mpaka tar 01/09/2012 na kuwa ingefika tar 02/09/2012 basi shughuli za mikutano ya hadhara zingeendelea.

Mnamo tar 29/08/12 Chadema iliandika barua ya kutaarifu kuendelea kwa mikutano tena na katika barua hiyo mikutano ilitarajiwa kufanyika 02/09/2012 na 03/09/2012. Mnamo tar 01/09/2012 ndugu A.M Mwanyasi-SSP Kamanda wa polisi wa wilaya ya Mufindi aliandika barua yenye Kumb. Na Mfg/A.24/9/54 kuruhusu mikutano ya Chadema kuendelea.

Chadema kwa kuwa tulipewa barua hiyo, tulianza shughuli za matangazo sehemu mbali mbali za jimbo la Mufindi kusini na maandalizi mengine kuhusu kulipia maeneo ya malazi kwa wanachama na viongozi mbali mbali waliopo kwenye msafara.

Masaa matatu baadaye, kama saa sita na kenda, nikapigiwa simu na kamanda wa polisi kuwa nifike pale kituo cha polisi cha Mafinga. Baada ya kufika hapo nikiwa na maafisa wengine wa chama, tukaelekezwa kuelekea ofisi ya OCD. Huko Kamanda wa Polisi wa wilaya akatupa barua nyingine yenye Kumb. Na Mfg/A.24/9/55 ikiwa na kichwa chenye maelezo ya kutaka kusitisha

mikutano ya Chadema, sababu ikiwa ni kuwa zoezi la sensa lilikuwa limeongezewa muda wa siku nyingine tatu. Kwa barua hiyo, Chadema tulifedheheshwa sana. Tulimsihi kuwa tayari kuna timu ya matangazo imeshasambaa sehemu mbali mbali na inaendelea na matangazo kwa wananchi; ajaribu kuona namna ya kutotuzuia lakini hakukuwa na mafanikio. Tuliamua kusitisha mazungumzo kwa muda mpaka pale tutakapojadiliana na viongozi wa kitaifa ambao wengine kati yao walikuwa wamesha wasili mjini Mafinga ambako ndiko makao makuu ya wilaya ya Mufindi.

Baada ya kuajdiliana na viongozi wa kitaifa na kwa ushauri na kamati kuu taifa, tulikubaliana kuwa tuendelee na mikutano kama kawaida kwa kuwa taarifa zilionyesha kuwa tume ya Sensa ilikuwa imetoa tangazo la kuwa wale wote wasiohesabiwa ndio wawatafute maafisa wa Sensa tofauti ya ilivyokuwa pale awali. Zaidi ya yote, siku hiyo, kulikuwa na mikutano ya CCM na mingine ya dini iliyokuwa ikiendelea maeneo mbali mbali ya nchi. Tukatafuta vielelezo vyote vya kuonyesha kuwa CCM na baadhi ya dini wanaendelea na mikutano katika maeneo mbalimbali na pia mikutano yetu isingeweza kuathiri shughuli za Sensa kama ilivyokuwa imedaiwa na jeshi la polisi.

Mnamo saa moja jioni tulirudi na kufanya kikao kingine na jeshi la Polisi, tukiambatana na Maafisa wengine wa Chadema taifa. Baada ya Muda mrefu wa mvutano, tuliachana bila ya maridhiano yeyote. Na kwa kuwa kulikuwa na sinto fahamu yeyote, kulikuwa na kila dalili kuwa jeshi la polisi lingetumia nguvu kubwa kuhakikisha kuwa mikutano ya chadema haiendelei. Chadema tulitambua hilo na kwa kuwa hatukutaka pia kuleta madhara kwa raia wa Tanzania tuliamua kurudi na kufanya tena kikao cha ndani kuona nini kifanyike. Mnamo saa nne usiku tukakutana tena kama kamati ya Chadema na tukakubaliana kuwa tufanye shughuli za ndani za Chama badala ya kufanya mikutano ya hadhara kama ilivyokuwa hapo awali. Siku ya 02/09/2012 timu ya maandalizi kuona ni ofisi zipi zifunguliwe ikawasili pale Nyololo.

Nimeandika hivi ili kila mtu atambue kuwa huu ndio ukweli ambao Marehemu Daudi Mwangosi alikuwa angependa kuufahamu. Kumbukeni kuwa kulikuwa na mvutano kati ya Chadema na Polisi kuwa ni nani alikuwa na haki zaidi kisheria ya kumsikiliza mwenzake. Kwa wale ambao wanahusika na kusimamia ofisi mbali mbali, katika taasisi mbali mbali. Tuone ni namna gani jeshi la polisi liliendesha shughuli zake kabla ya tukio hili. Ndugu zetu, ni ofisi gani ambayo inatoa maamuzi ya kufanya kitu fulani tena kwa maandishi halafu ndani ya masaa machache yasiyozidi masaa matatu inatengua maamuzi iliyoyafanya hata kama ni kwa maandishi?

Hapa tunalaumiana kwa sababu maamuzi yaliyofanywa na jeshi la polisi ndiyo yaliyosababisha kifo cha ndugu Mwangosi. Kama ingekuwa vinginevyo basi kusingetokea kilichotokea. Tena wazi wazi Chadema walikuwa wamesha fanya ufunguzi wa ofisi ya tawi na sasa mahali ambapo Mwangosi alifariki ilikuwa ni ofisi ya Kata ambapo viongozi wa Chadema walikuwa wanatia saini kuwa wamefika katika kata hiyo na wamefanya ufunguzi wa ofisi ya tawi na baada ya hapo ilikuwa ni kutoa nasaha kwa wanachama wa Chadema kabla ya kuwatawanyika.

Watanzania wengine wanailaum Chadema kuwa kwa nini ilishindwa kufuata amri ya Polisi? Naomba niwakumbushe kuwa hapo awali niliwaeleza kuwa Barua ya 28/08/2012 ya Polisi yenye kumb. Na Mfg/A.24/52 ilikuwa inazuia mikutano ya Chadema kuendelea kwa sababu zoezi la Sensa lilikuwa linaendelea toka 28/08/2012 mpaka 01/09/2012. Chadema walikubaliana na hilo na wakafanya shughuli za kukijenga chama kwa kuuza kadi na kuwahamasisha wananchi kujiunga na Chadema.

Pili, barua ya 01/09/2012 ya Polisi yenye kumb. Na Mfg/A.24/54 inaijibu barua ya Chadema ya 29/08/2012 kuruhusu mikutano ya hadhara iendeleo lakini tena kwa maajabu ya kiuendeshaaji wa ofisi, siku hiyo hiyo 01/09/2012 barua nyingine ya Polisi inaitaka Chadema isitishe shughuli za mikutano ya hadhara kwa kisingizio kuwa zoezi la Sensa limeongezwa muda. Ni uonezi gani huo.

Rasimu ya kitabu sio kitabu © 2014 Justin Mpotwa

Hata hivyo yalifanyika mazungumzo na Polisi ya kutaka kuwaonyesha kuwa ni namna gani serikali inafanya upendeleo. Tuliwathibitishia kuwa zoezi la Sensa lilikuwa halifanyiki kama ambavyo lilikuwa linafanyika hapo 28/08/2012 mpaka 01/09/2012 kwani wakati huu ilikuwa ni wajibu wa yule ambaye hajahesabiwa kwenda kwa hiari yake kuripoti kwa maafisa wa Sensa. Zaidi ya yote, tulilithibitishia jeshi la Polisi kuwa kulikuwa na mikutano ya dini na mengine ya kisiasa iliyokuwa ikiendelea sehemu mbalimbali za nchi hii na tukaliuliza jeshi hilo kuwa Chadema walikuwa na makosa gani kufanya mikutano hiyo.

Hata hivyo baada ya kuona kuwa kulikuwa hakuna maridhiano ndani ya kikao kile, Chadema tulikaa kikao kingine ili kutafakari hatua madhubuti ya kufanya na tukaona kuwa tusitishe mikutano ya hadhara na tufanye shughuli za ndani za chama. Mwangosi aliuawa wakati wa ufunguzi wa ofisi za chama na mikutano ya ndani ya chama. Mikutano ya ndani haingiliwi na Jeshi la Polisi. Nani kati ya Chadema na Polisi wanamakosa?

Huu ndio ukweli ambao Mwangosi alikuwa akiutafuta. Na tungependa wananchi wenzetu muutambue na muupime na muone nani alikuwa sahihi na ni nani alikosea?

V

Katikati ya Amri kutoka Dola

“Aliendelea Kutimiza Wajibu Wake”

Wakati ilipotolewa amri ya Kututawanya kwa mabomu, bomu la kwanza lilipigwa na mengine mengi yakafuata. Hakuna aliyekuwa na uwezo wa kuendelea kukaa pale chini. Kila mmoja alikuwa anatafuta ni wapi ingekuwa salama yake. Mimi na wenzangu tulikimbia mbali sana kutoka pale tulipokuwepo, ofisi za Chadema.

Nimeangalia video ambayo inaonyesha nini kilikuwa kinatokea. Ni kweli inasikitisha. Mwangosi alikuwepo akikisubiri kifo chake akiwa ameshika kamera yake na laptop yake kifo kikamjia pale pale bila hata huruma. Aliendelea kupiga picha ili aujulishe ulimwengu juu ya kinachoendelea katika Demokrasia ya Tanzania. Tutampata wapi Mwangosi ambaye amekufa mikononi mwa polisi chini ya maamuzi ya Polisi. Ee Mungu tunakushukuru kwa kutupa kijana Shujaa ambaye hakuiogopa amri ya Dola yenye kukandamiza haki za wanyonge.

Ushujaa aliouonyesha Mwangosi ni ushujaa wa watu waliopitiliza kupenda. Alipenda hata mauti ya Bomu la Polisi. Aliwapenda watanzania hata akawa tayari kuyatoa maisha yake kwa kumwaga damu. Ukiangalia picha zinazoonyesha namna ambavyo mwili wake umelala pembezoni mwa polisi mmoja aliyekuwa akimtetea ambaye naye alivunjwa miguu yake inasikitisha sana.

Kwa namna ya pekee, ningependa kumtunuku zawadi ya kumbukumbu yule askari aliyekuwa akimtetea Marehem Mwangosi. Nina amini kuwa hata katika vyombo vya dola kuna watu wengi wenye moyo wa huruma. Nchi yetu inawatu wengi sana wanaoitakia mema amani na demokrasia yetu. Wote kwa namna ya pekee tunawashukuru sana. Mara kadhaa dola inatoa amri ambazo zinahatarisha mstakabali wa uhai wa wananchi lakini pia vile vile mstakabali wa amani. Hata hivyo kunajitokeza watumishi wa dola ambao wanawaonea huruma watanzania wengine. Tunapenda kuwashukuru.

Ningependa kuwatia moyo watumishi wa umma na wa vyombo vya dola. Kuna wakati mnapewa amri zisizolitakia mema taifa letu lakini aidha mnazipuza au mnatafuta namna ya kutotekeleza

kama ilivyokusudiwa. Kwa namna ya pekee tunatambua mchango wa mahakama ya Tanzania. Kipindi cha hivi karibuni tumeshuhudia mahakama ikitenda haki. Wantanzania na hasa wanaharakati tunawashukuru na tunaendelea kuwapa moyo na kuwaomba msituache kwani tunatambua uwepo wa watu wasiotutakia mema sisi. Dhamana mliyo nayo kwa maisha yetu na kwa haki zetu ni kubwa sana.

Kwa namna ya pekee ningependa kuwashukuru waandishi wa habari ambao walikuwepo pale siku ya tukio. Kijitabu hiki kiwe ni sehemu ya kuwakumbuka na kuutambua mchango wenu. Tumeutambua mchango wenu na tunatambua kuwa wote nyinyi mlikuwa katika hatari sawa kabisa na ile aliyokuwa nayo Daudi Mwangosi. Tunatambua kuwa kama endapo mngekuwa mlimwacha Mwangosi peke yake, basi hata zile picha zinazoonyesha namna alivyouawa tusingezipata. Mpaka sasa kunarekodi nyingi zinazoonyesha uwepo wa mazingira ya hatari sana kwenu. Ni jambo la sisi watanzania kuwashukuru na kuwaombea mwendeleo na moyo mliokuwa nao.

Tunachokiomba ndugu zetu waandishi ni kuwa katikati ya mazingira ya hatari, msituache. Tunawahitaji sana na kwa kuwa mnaendelea kuwa watetezi wetu tutaendelea kuwashukuru. Kalamu zenu ziendeleo kuandika yale maovu yanayotokea katika jamii bila kujali itikadi za vyama vya siasa, dini, ukabila, ukanda, rangi n.k. Kuna tetesi kuwa kati yenu kuna baadhi yenu wamekuwa wakikiuka maadili ya kazi yenu. Wapo wanaoandika habari za uongo, wapo wanaochukua rushwa na wengine hata kudiliki kuwagawa watanzania kwa misingi ya itikadi mbali mbali. Tunaomba waache. Kazi yenu ni moja ya mihimili mikuu ya nchi. Kazi yenu ikiyumba, Tanzania inayumba. Msiiyumbishe Tanzania.

Vile vile, fursa ya kuandika kijitabu hiki iwe pia kuvishukuru vyombo mbali mbali vya Habari. Sisi watanzania tunavishukuru vyombo hivyo kwa kuwa tunatambua kuwa vimetuleta nuruni. Wamiliki wa vyombo hivyo pia wamejitahidi kwa namna ya pekee kutoingilia uhuru wa vyombo

vya habari wanavyovimiliki. Tunatambua kuwa wamiliki wa vyombo vya habari pia mnaitikadi mbali mbali ambazo pengine zingewasukuma kuingilia uhuru wa vyombo vyenu, hata hivyo wengi wenu mmejikaza na kuviacha vyombo vyenu kuwa huru. Kijitabu hiki kiwe ni sehemu ya kumbukumbu yetu kwenu.

Hatutaacha pia kuwashukuru wanaharakati wote wa haki za binadamu, waliondani ya vyama vya siasa, mashirika binafsi, dini na madhehebu mbali mbali, taasisi binafsi na za kiserikali na wale wanaharakati binafsi ambao wao kila siku wanafanya kila liwezekanalo kuhakikisha watanzania wanapata haki zao za msingi na wanatimiziwa mahitaji yao.

Tunawanaharakati waliopo mashuleni na vyuoni ambao wao kila siku wanahakikisha kuwa wanafunzi wanapata elimu bora. Tunawanaharakati waliopo mahospitalini na kwenye vituo vya afya ambao wao kila siku wanahakikisha kuwa wagonjwa wanapewa matibabu yanayostahili. Tunawanaharakati pia wanaotetea haki mbali mbali za wanawake, watoto, wazee, wastaafu, walimu, madaktari, vijana, wafanyakazi, wakulima, waajiriwa na waajiri. Wote hawa ni wanataka kuhakikisha kuwa wanaleta usawa kati ya watawala na watawaliwa. Kijitabu hiki ni sehemu ya kumbukumbu yetu kwenu.

Ningeomba watanzania wote tuwaheshimu wanaharakati na wengine wote waliotajwa katika kijitabu hiki kwani wao ndio watetezi wa sisi tusio na sauti. Bila wao, mambo, pengine na kwa hakika yangekwenda mrama. Tujichunguze sisi kama watanzania, tusio na sauti je, kwa namna ambavyo kumekuwa na msugvano wa wazi kabisa kati ya watawala na hawa wanaharakati, kama si kwa msukumo wanaounyesha hawa wenzetu wanaharakati, hali ya Tanzania ingekuaje

Kwa namna ya pekee ningependa kutoa mwaliko kupita kijitabu hiki kwa wale wote waliopolekwa shule kwa kodi za wananchi kuwa sasa imefika wakati wa kuamka na kuanza kuzipigania haki za wanyonge. Nitalizungumza hili zaidi katika mada inayofuata. Dunia inahitaji wapigania haki waliotayari kutimiza wajibu wao kikamilifu kwa mujibu wa sheria bila ubaguzi.

V

KATIKATI YA WAHITAJI

“Aliwapigania”

Nimeeleza namna tulivyotawanyishwa na tukapoteana kwa kukimbia kimbia huku na kule. Kuna wengine walipoteza simu, kunawengine walikutana na virungu vya polisi na mambo mengine mengi. Katika mada hii nitaanza kwa kueleza nini kilitokea mara tu ya Mwangosi kuuawa.

Ilichukua takribani dakika tano toka nikimbie eneo la tukio. Nikawa nawaza nifanyeje? Kwa kuwa nilikuwa nimeacha gari niliyokuwa ninaitumia siku hiyo, basi ilinibidi nifanye ushujaa kurudi pale kwenye tukio. Nilitafuta njia za uchochoroni nikatoa alama zote za Chadema nilizokuwa nimezivaa nikiwa naamini pengine Polisi wametawanyika kututafuta. Mara nikatokezea kwenye barabara inayoelekea eneo la tukio. Nilipotokea tu barabarani nikakutana na kikundi cha watu ambapo mmoja ya walikuwepo kwenye kikundi kile alikuwa mzee mmoja ambaye alikuwa analalmika kuwa Polisi wamemuua mwandishi wa habari. Huyo mzee kwa jinsi nilivyomuona alikuwa ni mkazi wa Nyololo. Sikuamini maneno yale na nikaelekea moja kwa moja eneo la tukio.

Ninapofika pale, nikakutana na mama mmoja ambaye yeye alishuhidia moja kwa moja nini kilikuwa kinaendelea akawa akilalamika kuwa Polisi wamemuua mwandishi wa habari. Na kwa kututhibitishia kuwa ni Polisi waliofanya kile kitendo, akatuambia kuwa ameona Polisi wakifukia kitu fulani mithiri ya nyama eneo ambalo Mwangosi alifia. Akawa anatuonyesha eneo lenyewe. Mmoja wetu akafukua kwa mikono na ndipo tukauona utumbo wa Mwangosi. Jaribu kupata picha, unafukua unauona utumbo wa binadamu mwenzi uliyekuwa naye takribani dakika tano zilizopita akiwa mzima wa afya, akiwa anatekeleza majukumu yake.

Yule mama alienda mbali zaidi kwa kusema, “*wamemuua mwandishi wa habari, sasa sisi tutapata wapi habari?*” Huu ndio msingi wa ninachoenda kukizungumzia. Marehemu alikufa akiwatumikia wahitaji. Jamii yetu hakuna kitu kikubwa inachokiitaji zaidi ya kuelimishwa. Na ili mtu yeyote aweze kuelimishwa hana budi kupata taarifa. Ibara ya 18, ya katiba yetu inasisitiza

jambo hilo kwa kusema kila mtu anao uhuru wa kupata taarifa na habari lakini pia ana uhuru wa kutoa tarifa pasipokuwekewa mipaka yeyote.

Sasa kwa kuuawa Mwangosi, akiwa anawatumikia wahitaji tunajifunza nini? Je, haki yake imetimizwa? Ni hatua gani za kisheria zimechukuliwa kuwashughulikia waliohusika? Mpaka sasa kuna mambo makubwa mawili yanayonisikitisha. Jambo la kwanza ni namna ambavyo kesi ya muuaji wa Mwangosi inavyoendeshwa. Sitaki kuingilia uhuru wa mahakama bali nasema tu hitaji la Mwangosi huko aliko halitimizwi.

Jambo la pili ni kuona kana kwamba lile tukio la Mwangosi kuuawa liliongeza sifa kwa ndugu Kamuhanda aliyekuwa kamishna wa Jeshi la Polisi mkoa wa Iringa wakati wa kifo cha Mwangosi. Mwangosi aliuawa hatua chache toka lilipokuwepo gari la Mkuu huyo wa Jeshi la Polisi. Licha ya tume ya haki za binadamu kumtaja kuwa alikiuka sheria na taratibu za kazi yake lakini pia alishindwa kukitendea haki Chadema na zaidi ya yote, wakati Mwangosi anauawa kuna mwandishi wa habari wa gazeti la Tanzania Daima alimfuata na kumgongea dirisha la gari na kumthibitishia kuwa aliyekuwa anapigwa na Polisi alikuwa ni mwandishi naye hakuchukua hatua. Lakini bado kapandishwa cheo.

Mambo haya mawili yananitilia wasi wasi ju ya umakini na umahiri wa Jeshi la Polisi. Nimeandika haya kwa uchungu na kwa kuwa mimi ni shahidi mmoja wapo wa yote yaliyotokea kabla, wakati na baada tu ya tukio. Zaidi ya yote, mimi ndiye niliyekuwa ninaweka sahihi kwenye barua tulizokuwa tunawatumia Polisi, kwani wakati huo nilikuwa katibu wa wilaya. Sitakuwa ninamtendea haki Mwangosi kwa kutosema chochote lakini zaidi ninaomba niliyemtaja katika kijitabu hiki asinieleme vibaya. Ni kuwa tu ninatimiza wajibu wangu kuitafuta haki ya Mwangosi. Na nimeeleza kuwa ninaitambua hatari iliyopo mbele yangu lakini nipo tayari kuikabili.

Kwa familia ya Mwangosi, tunawaomba muwe wavumilivu katika kipindi kigumu mnachokipitia, hasa ikiwa ni mwaka mmoja tu toka kifo cha ndugu yetu, kaka yetu na kiongozi wetu. Tunatambua kuwa mmesononeshwa sana na tukio lile lakini kwa namna ya pekee tunaomba kuwashukuru kwa uvumilivu mnaoendelea kuuonyesha.

Tunaomba wanaohusika na kila haki ya Mwangosi watambue kuwa Mwangosi hatatoka kamwe katika fikra zetu. Tutaendelea kumkumbuka na kumshukuru kwa yale yote mema aliyotutendea. Ni kweli kabisa Mwangosi alikuwa kiongozi mwadilifu nasi tunajifunza kutokana na uadilifu wake. Waitendee haki familia ya Mwangosi badala ya kuwasifia waliotenda unyama ule na zaidi ya yote kuwapandisha vyeo waliohusika. Hii ni kama kuikejeli familia ya Mwangosi na zaidi ya yote ni kuiumiza familia yake. Nilisema pale awali kuwa Serikali ya Mkoa wa Iringa pia ionyeshe kuwa inatambua mchango wa Mwangosi badala ya kuonyesha wazi wazi kukishabikia kile kitendo kama mmoja wa Mawaziri anayetoka mkoa wa Iringa alivyofanya pale Bungeni.

Mwisho ningependa kuwatia moyo, Ndugu wote, Marafiki wake na wale waliowahi kusoma, kukutana na kufanya kazi na Marehemu. Ni jambo la heri sana kukutana na Shujaa Mwangosi. Kwani inatufanya wanaharakati tupate nguvu zaidi. Mimi kwa mfano hata kuandika kijitabu hiki, ni Mwangosi aliyenipa moyo. Nimeendelea kuwasiliana naye kifikra na hata nikaona sina budi kuandika kijitabu hiki hata kama mbeleni kuna hatari itakayonikabili. Mwangosi ni rafiki yangu wa karibu hata kama sikuwahi kufanya nae kazi ila kwa kuwa nimekutana naye dakika takribani tano nimeamua awe rafiki yangu wa milele hata huko aliko.

Sijui wewe msomi mwenzangu, uliyesoma kwa kodi za wananchi na bado unakaa kimya ukiwaona watanzania wenzako wakiteseka kwa kukosa haki zao na wakati mwingine unashiriki katika kuzikandamiza haki hizo unajisikiaje? Vijana, tuamke tuipiganie haki ya watanzania wenzetu kama ambavyo alifanya Mwangosi kwa wahitaji. Mimi leo nimetoa mchango wangu mdogo kwako wewe uliyesoma kijitabu hiki, kwani ninaamini ulikuwa ukiihitaji sana

Rasimu ya kitabu sio kitabu © 2014 Justin Mpotwa

kuufahamu ukweli nilioueleza. Wewe nawe tafuta watanzania wanahitaji kufanyiwa nini kutoka kwako, uwatendee kwa kadri ya mahitaji yao. Wape msaada wa kila linalowezezekana ili mwisho wa siku tuipate Tanzania iliyostaarabika, Tanzania yenye Amani na Upendo na si Amani na Utulivu peke yake.